**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WERUWERU ………

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**
**SHULE YA SEKONDARI WERUWERU**

S.L.P. 575

**MOSHI**

Nambari ya simu: 0768315332/0759659681
Email:weruweru23@gmail.com

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………………
…………………………………………………………….
S.L.P …………………………………………………
…………………………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WERUWERU HALMASHAURI YA MOSHI MKOA WA KILIMANJARO MWAKA ……..**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Weruweru mwaka…….. tahasusi ya ………………, Shule ya Sekondari Weruweru ipo umbali wa kilometa kumi (10) kutoka mji wa Moshi. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **cha maili sita nauli shilingi mia Sita (600**).Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe........................ Mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………... Mwanafunzi akichelewa kuripoti ndani ya kipindi hicho nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.**

## A. MAAGIZO YA FEDHA:

Binti yako atapaswa kuchangia **jumla ya shilingi 80,000/= (Elfu themanini tu) kwa mchanganuo uliooneshwa katika jedwali hapo chini kwa jina la Mkuu wa Shule kupitia akaunti namba 40301100091 Weruweru Sekondari** iliyopo **Benki ya NMB** tawi lolote , kumbuka kuandika jina la mwanafunzi, kidato chake na tahasusi (combination ) sehemu ya ujumbe. **FEDHA TASLIMU HAZIPOKELEWI SHULENI**. Mwanafunzi aje na Nakala ya hati ya malipo. **NAKALA HALISI (original Bank pay in slip).**

### 1.1 MICHANGO MBALIMBALI

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 2. 0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI MWANAFUNZI ANAPOKUJA SHULENI :-

i. Aje na mashati mawili meupe yenye mikono mifupi aina ya ”**TOMATO”**
ii. Aje na sweta ”V” shape shingoni ya rangi ya dark blue (NAVY)
iii. Aje na hijabu ya rangi nyeupe kwa ajili ya darasani na rangi ya **”dark blue”** kwa ajili ya kuvalia nguo za kushindia. **Hii ni kwa Waislamu tu**.
iv. **SARE YA MICHEZO** ni truck suit nyeusi yenye mistari meupe pembeni koti la truck suit lisiwe na kofia.
v. **VIATU VYA SHULE** ni vyeusi vya kufunga na kamba kuanzia matundu sita hadi nane vyenye visigino vifupi**;(visiwe aina ya FACEBOOK wala aina ya buti)** na raba nyeusi za michezo ni muhimu.zingatia hili kinyume na hapo mwanafunzi atarudishwa.
vi. Aje na soksi nyeupe jozi nne (04),simple shoes nyeusi za kufunika (jozi moja), kandambili jozi moja **(asije na yeboyebo),** khanga, gauni la kulalia na taulo.
vii. Aje na ” poly – neck” nyeusi au nyeupe kama ana matatizo ya kifua.
vii. Aje na magauni mawili marefu yanayovuka magoti ya rangi ya “Pink” (mshono wa solo) yenye mikono mifupi nakola **“baby colar**” na suruali yake Isiyobana Kama nguo za hushindia. **Nguo nyingine haziruhusiwi** .
vii. T- shirt moja rangi ya kijivu 180 “type ASH - GREY “ kwa ajili ya michezo. Ukishindwa kupata aina na rangi hiyo lipia kiasi cha **shilingi elf 12,000** kwenye **akaunti namba 40310005919 NMB Jina la Akaunti ni Weruweru Sec.Self Reliance Fund** na ataipata shuleni.

## 2.1. MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

i. Madaftari counter book 4Q yasiyopungua kumi (10), madaftari madogo ya msomi (10) kwa ajili ya mazoezi.
ii. **Ream** mbili (02) za karatasi aina ya Rotatrim/daouble A/ Top copie/NO1;
**iii.** Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kutoka TIE (Tanzania Institute of Education**). Kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya Jiografia waje na kitabu cha ramani na picha (current coloured mapsheet and photography by Talezo)**
iv. “mathematical set”, rula ndefu, kalamu za wino za kuandikia, penseli, kifutio, “stepler machiner” “graph pad” na Scientific Calculator;(**aina ni CASIO fx-991 ms from Thailand)**
v. Godoro linakodishwa shuleni kwa gharama ya **Shilingi 15,000.00** kwa mwaka Alipie kwenye akaunti **Namba 40301100091 Jina la Akaunti Weruweru Secondary School. Asijie na godoro.**
vi. Shuka za kulalia mbili (02), Blanketi la kawaida “student size”, mto na foronya mbili, chandarua nyeupe ya duara au mstatili na “bed cover” shuka la kutandika juu ya kitanda moja (01) la rangi ya “Pink” ili kuleta ufanano
vii. Nguo za ndani za kutosha asije na “boxer”

viii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate) na nakala ya cheti cha matokeo yake ya kidato cha nne (Result slip).

ix. Taulo spesheli (Pedi)

x. Vyombo vya chakula. Aje na kijiko tu, sahani na kikombe atapata shuleni.

xi. Ndoo moja (01) ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 10 kwa matumizi yake binafsi na ndoo moja (01) yenye ujazo wa lita 20 kwa ajili ya matumizi ya shule (yenye rangi ya"Green")

xii. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kuja na manukato ya aina yoyote (perfume/deodorant) pia wasije na mafuta ya kupaka yenye harufu kali

xiii. Aje na toilet paper ya kawaida na siyo wipes wala tissue paper.

xiv. Kila mwanafunzi aje na fagio moja (01) fupi la chelewa na brush ngumu fupi ya kusugua sakafu (**scrubing brush 02**) **tafadhali zingatia ubora**

**xv.** Kila mwanafunzi alete kifaa kulingana na mchepuo wake kama ifuatavyo. **HGE – FAGIO LA BUIBUI**, **HKL na ECAc** – **JEMBE LILONOLEWA NA MPINI WAKE, HGK – "SOFTBROOM"FAGIO LAINI LENYE MPINI, PCB – BRASHI LA CHOONI** "**toilet brush 1". EGM –"LONG SCRUBING BRUSH"** (**Srubing brush ndefu yenye mpini**), **BUACM – REKI LA CHUMA LENYE MPINI , EBUAC – FYEKEO LILILONOLEWA VIZURI, PCM – SABUNI YA MAJI LITA TANO AU SABUNI YA UNGA NDOO NDOGO (Hii ni kwa ajili ya kufanyia usafi) .**

xvi. Aje na sanduku dogo la bati (size ya kati linaloweza kuingia katika uvungu wa kitanda chake) na kofuli lake liwe imara. Asije na sanduku lenye material ya nguo/ngozi "Suit case" hatutalipokea. Asije na begi lenye "Charge" (USB BAG) smart watch" au kifaa chochote cha electronics kinachohitaji kutumia umeme.

### 2.3. <u>SARE ZA SHULE</u>

Sare ya Shule ya Sekondari Weruweru ni Sketi mbili (02) zenye rangi ya "darkblue" (SUIT MATERIAL) yenye "V" shape mbele isiyo ya kubana ndefu yenye kuvuka magoti muundo wa solo. Zingatia ubora wa kitambaa mshono na rangi uliyoelekezwa ili kuepuka utofauti. **Ukishindwa kushona na kupatia mshono ulioelekezwa lipia kiasi cha Tshs 40,000/= (Elfu arobaini tu)** kwenye **akaunti 40310005919 NMB Jina la Akaunti ni Weruweru Sec.Self Reliance Fund** atapewa shuleni.

**NB: Aje na sketi ya shule aliyokuwa anaitumia akiwa kidato cha nne atakayo vaa wakati akisubiria kushonewa sare ya shule**.

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu ,"line" au "charger" shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Ni marufuku mwanafunzi kusuka nywele.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kuondoka katika eneo la shule bila kibali cha Mkuu wa Shule / utoro
xix. Kulala wawili katika kitanda kimoja.

## 4.0. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU.

**Viambatisho vifuatavyo mwanafunzi aje navyo siku ya kuripoti shuleni;**

i. Hakikisha binti yako anapimwa na daktari na kujaziwa Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali / imeambatanishwa (**kiambatanisho Na1);**
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi imeambatanishwa **(kiambatanisho Na 3) "Information sheet"**
iii. Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule /imeambatanishwa; **(kiambatanisho Na 2)**
iv. **Hakikisha mwanao ana BIMA YA AFYA kama hana aje na shilingi Elfu hamsini na nne mia tano (54,500) atakatiwa bima shuleni.**

## 5.0. MENGINEYO KWA UMUHIMU

**(i)** Wazazi /wageni kutembelea wanafunzi.

Wazazi hawaruhusiwi kuonana na watoto wao wawapo shuleni. Hii itawasaidia kutumia muda wao vizuri zaidi katika kujisomea. Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kufika Shuleni na kutaka kuwaona wanafunzi na hii huwasumbua na kuathiri utendaji wao kimasomo.

**Mwanafunzi asifike shuleni siku za week-end wakati wa kuripoti kwani hatapokelewa.**

**N:B: Shule ina utaratibu wa kuwa na vikao vya wazazi mara moja kwa mwaka hivyo kwa mwaka huu kikao kitakuwa tarehe 30/08/2025**

**(ii)** Mwanafunzi haruhusiwi kuja na dawa zake binafsi kwani atahudumiwa katika Zahanati ya shule **lakini ikiwa amepewa dawa na Daktari atatakiwa kumkabidhi Muuguzi wa shule ambaye atafuatilia matumizi yake.**

**(iii)** Ni vyema mzazi ukahakikisha mtoto anapokuja shuleni amechukua tahadhari zote za kiafya.

**(iv)** Shule inajitahidi kuwapa wanafunzi chakula bora na cha chukutosha hivyo mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na chakula cha aina yoyote.

**(v)** Niwazi kuwa mwanafunzi lazima apewe pesa za matumizi ni wajibu wa mzazi au mlezi kumpa binti yake kiasi cha pesa kwa ajili ya mtumizi madogomadogo kama vile, sabuni stampu, bahasha nk sio busara kumpa mtoto pesa nyingi kwani hii husababisha wizi, mashindano, ubaguzi, tabaka, ugomvi na urafiki usiokuwa na msingi. Hata hivyo tunashauri umfungulie

mwanao akaunti au aje na shilingi **10000/=** kwa ajili ya kufungua akaunti akiwa shuleni ambayo utakuwa unaitumia kumtumia mwanao fedha ya matumizi **(NMB/CRDB)**

**(vi)** Mzazi anatakiwa kumsafirisha binti yake wakati wa kuja shule na anapo rudi nyumba wakati wa Likizo. Ni muhimu fedha za usafiri zitumwe mapema mara baada ya kupokea taarifa wakati utakapo fika ili usafiri wa pamoja upangwe na shule.

**vi) Wanafunzi hawaruhusiwi kwenda Nyumbani wakati wa masomo isipokuwa:**

(a) Ametumwa / amepelekwa na Shule.

(b) Wazazi /mlezi wake waje kumchukua kukitokea shida kubwa nyumbani mfano Kifo cha baba mzazi, Mama mzazi au mlezi wake anayetambulika kisheria (Wale tu waliojazwa katika taarifa zake binafsi)

(c) Ni lazima waje na barua yenye saini na muhuri wa Mtendaji wa kijiji / mtaa kudhibitisha tukio hilo.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0759 659 681.**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0754 347 977.**
- **Mwandamizi Taaluma 0672 666 804**
- **Mwandamizi Malezi 0714 487 370**
- **Namba ya Shule 0768 315 332**

Mara upatapo fomu hii unaweza kutuma ujumbe wa kuomba kuunganishwa kwenye group la wazazi kwenda namba **0754347977 ni muhimu**

**HITIMISHO:**

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto waendelee na wapate kile walichokifuata hapa shuleni Weruweru , yaani **ELIMU.** Msisisitizo wa Bodi ya Shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha asilimi **60%** au zaidi katika kila somo. Sheria zote hizo zinalenga kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masoma yake.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA WERUWERU SEKONDARI;**

**Saini ya Mkuu wa Shule …..................................**
**Jina la Mkuu wa Shule ROSALIA T. FRIMINI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………………….**

.

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**

**WERUWERU SECONDARY SCHOOL,**
**P. O. BOX 575,**
**MOSHI.**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical Officer in respect of all form entrants.

Full Name……………………………………………………………………………………………………..
Age…………………………………………………………………………………………………………
Blood count (Red and White) ……………………………………………………………………..
Stool Examination…………………………………………………………………………………..
Urine analysis and Pregnancy test …………………………………………………………………..
Syphilis test …………………………………………………………………………………………….
T.B. Test …………………………………………………………………………………………………….
Eye Test …………………………………………………………………………………………...............
Ears ……………………………………………………………………………………………………………
Chest ………………………………………………………………………………………………………….
Spleen …………………………………………………………………………………………………...
Abdomen ………………………………………………………………………………………………….

ADDITION INFORMATION: e.g. physical or chronic family diseases etc.
…………………………………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………….

I certify that the above is fit to pursue studies
Signature …………………………………………………………..
Designation …………………………………………………….
Section ……………………………………………………………
Date …………………………………………………………………

STUDENT: You must bring this completed form when you come to School. No student will be allowed to enroll without certificate of physical fitness.

**HEADMISTRESS**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**

Shule ya Sekondari Weruweru,
S.L.P. 575,
**MOSHI.**

Tarehe **..........................**

**HATI YA UTII WA SHERIA**

Mimi Bwana / Bibi........................................................................ Mzazi / Mlezi wa........................................................... nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa katika Maagizo kwa wazazi na nazikubali Sheria hizo na nitashirikiana na Shule kuona kuwa mwanangu anazizingatia kwa manufaa ya Umma.

Mimi ……………………………….. Binti wa Bwana / Bibi ………………………………………….. Nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali Sheria hizo. Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa naelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma.

……………………………………………. ……………………………………….

**SAINI YA MWANAFUNZI** **SAINI YA MZAZI**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA PRIME**
**MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**
**WERUWERU SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 575, MOSHI**

**STUDENT INFORMATION SHEET:-**

(This form is to be completed by form five and student transferred to the school. Parts A, B and C to be completed by the student)

**A: PERSONAL PARTICULARS:**

NAME: …………………………………………………………………………………………………………………………………
DATE OF BIRTH: ……………………………………………………………………………………………………………………
TRIBE: …………………………………………………………………………………………………………………………………
RELIGION: ……………………………………………………………………… DENOMINATION……………………………………
FATHER'S NAME: ………………………………………………………………… OCCUPATION………………………………………
MOTHER'S NAME: ……………………………………………………………… OCCUPATION ………………………………………
GURDIAN'S NAME: ……………………………………………………………… OCCUPATION ………………………………………
NUMBER OF SISTER'S: ……………………………………………………… NUMBER OF BROTHERS ……………………
FARTHER'S TELEPHONE NUMBER: ……………………………………… MOTHER'S TELEPHONE NO ……………………
HOME ADDRESS: ……………………………………………………………………………………………………………………
ANY PHYISICAL/ MEDICAL DISABILITY ……………………………………………………………………………………

**B: SECONDARY EDUCATION:-**

……………………………………… SECONDARY SCHOOL: FROM …………………………… TO ……………………
……………………………………… SECONDARY SCHOOL: FROM …………………………… TO ……………………
……………………………………… SECONDARY SCHOOL: FROM …………………………… TO ……………………

**C: PREVIOUS SECONDARY SCHOOL (IF TRANSFER TO THIS SCHOOL)**

NAME OF THE SCHOOL: ……………………………………………………………………………………………………………
ADDRESS: ……………………………………………………………………………………………………………………………
"I CERTIFY THAT THE ABOVE INFORMATION IS CORRECT TO THE BEST OF MY KNOWLEDGE"

……………………………………… ……………………………………………… ……………………………………………
**DATE** **NAME OF STUDENT** **STUDENT SIGNATURE**

**D: (TO BE COPLETED BY FORM CO –ORDINATOR):**

DATE OF ADMISSION TO THIS SCHOOL ………………………………………………………………………………………
DATE OF ADMISSION NUMBER ……………………………………………………………………………………………………
ADMISSION NUMBER ……………………………………………………………… YEAR ………………………………………………
FORM ADMITTED ………………………………………………………………………… YEAR ………………………………………………
DATE OF LEAVING SCHOOL ………………………………………………………………………………………………………
HIGHEST FORM REACHED …………………………………………………………………………………………………………
CSEE (FORM IV) EXAMINATION NO ………………………………………. ……………………………………………………
SIGNATURE OF FORM CO-ORDINATOR ………………………………… DATE …………………………………………………
SIGNATURE OF THE HEADMISTRESS ………………………………………. DATE …………………………………………………